



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAMLAKA YA MAJISAFI NA MAJITAKA DAR ES SALAAM
TAARIFA KWA UMMA

MHE. PROF. MBARAWA ASHUHUDIA TEKNOLOJIA YA KISASA YA UPIMAJI KINA CHA VISIMA

• AMPA MKANDARASI MIEZI MINNE KUMALIZA KAZI

Waziri wa Maji na Umwagiliaji Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa ametembelea mradi wa uchimbaji wa visima virefu vya Kimbiji na Mpera na kumtaka mkandarasi kumaliza kazi zilizobaki katika kipindi cha miezi minne kutoka sasa. Ziara hiyo ni muendelezo wa ziara za kutembelea miradi mbalimbali inayotekelezwa ya Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam (DAWASA) mara baada ya kuteuliwa kushika nafasi hiyo.

Akiwa katika ziara hiyo Mhe. Waziri aliweza kushuhudia teknolojia ya upimaji wa kina na ubora wa visima kwa kutumia kamera maalum inayoweza kurekodi urefu na kuonyesha vifaa vyote vilivotumika ndani ya visima hivyo vya kina kirefu. Visima vya Kimbiji na Mpera ni moja ya miradi ya kimkakati inayotekelezwa na Wizara ya Maji na Umwagiliaji kupitia DAWASA yenye lengo la kuongeza wingi wa maji katika eneo la huduma ya Mamlaka hiyo kutoka lita milioni 300 mpaka 720 zitakazotosheleza mahitaji katika eneo hilo hadi mwaka 2032.

Visima 20 vya Kimbiji na Mpera vina kina cha kati ya mita 435 na 625 huku baadhi vikiwa na uwezo wa kuzalisha maji kati ya lita 100,000 hadi 450,000 kwa saa. Kwa ujumla wake visima hivi vinatarajiwa kuzalisha maji lita milioni 260 kwa siku.

Tayari visima 19 kati ya visima 20 vimeshachimbwa kwa urefu tofauti. Mradi wa uchimbaji wa visima vya Kimbiji na Mpera unatekelezwa na Serikali ya Tanzania kupitia Mkandarasi NSPT ya Iran na Serengeti ya Tanzania kwa gharama ya Tsh. bilioni 19.8.

Kukamilika kwa visima hivi kutaimarisha upatikanaji maji katika maeneo ambayo hayakuwa na huduma nzuri ya majisafi na yale yasiyo na mtandao rasmi. Maeneo hayo ni pamoja na; Kigamboni, Kibada, Kisarawe II, Kongowe, Gongolamboto, Segerea, Pugu, Chanika, Chamazi, Charambe, Buyuni, Mbagala, Makangarawe, Tazara, Ukonga, eneo la viwanda la Barabara ya Nyerere, Uwanja wa ndege, Kiwalani, Mji wa Mkuranga Mkoani Pwani pamoja na baadhi ya vitongoji vyake vikiwemo Kisenvule na Kibamba .

Imetolewa na
Ofisi ya uhusiano wa Jamii